**JAMHURI YA MUUNGO WA TANZANIA**

**BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA**

**MTIHANI WA UALIMU DARAJA LA A**

**638** **VIELELEZO NA TEKNOLOJIA**

**Muda: Saa 3.** **Year: 2024**

---

**Maelekezo**

1. Karatasi hii ina Sehemu **A** na **B** zenye jumla ya maswali **kumi na manne (14).**
2. Jibu maswali **yote** kutoka Sehemu **A** na maswali **manne (4)** kutoka Sehemu **B**.
3. Sehemu **A** ina alama **arobaini (40)** na Sehemu **B** ina alama sitini **(60).**
4. Simu za mkononi **haziruhusiwi** ndani ya chumba cha mtihani.
5. Andika **Namba yako ya Mtihani** katika kila ukurasa wa kijitabu chako cha kujibia.

maktaba.tetea.org
TETEA


Find this and other free resources at: https://maktaba.tetea.org

**SEHEMU A (Alama 40)**

Jibu maswali **yote** katika sehemu hii.

1. eleza kwa kifupi mambo manne muhimu ya kuzingatia kabla ya kutengeneza vielelezo na Teknolojia kwa kufundishia wanafunzi wa Darasa la Pili.
2. toa hoja juu ya umuhimu wa kuzingatia malengo mahususi ya somo wakati wa kufaragua na kutengeneza zana.
3. chambua madhara manne yanayoweza kujitokeza kutokana na matumizi ya Vielelezo na Teknolojia visivyokidhi vigezo katika ufundishaji na ujifunzaji.
4. toa sababu za kuzingatia vipimo wakati wa kuchora michoro mbalimbali kwa ajili ya ufundishaji na ujifunzaji.
5. toa vigezo vinne vya kutathmini ubora wa vielelezo na teknolojia.
6. thibitisha kauli kwamba "Vielelezo na Teknolojia za kisasa vikitumika ipasavyo ni kichocheo kikubwa katika kuboresha zoezi la ufundishaji na ujifunzaji".
7. tetea kwa kutumia hoja nne juu ya kauli isemayo "Redio, redio kaseti, sauti zilizorekodiwa na kipaza sauti hutumika mara chache na walimu wengi katika ufundishaji na ujifunzaji kutokana na changamoto mbalimbali."
8. kubaliana na kauli kuwa "ni rahisi kutumia Vielelezo na Teknolojia maono katika ufundishaji na ujifunzaji kuliko makundi mengine ya Vielelezo na Teknolojia."
9. eleza kwa ufupi hatua nne za kutengeneza zana.
10. kwa kutumia hoja nne onesha namna ujaribishaji wa zana kabla ya kutumiwa darasani huongeza ufanisi wake katika ufundishaji na ujifunzaji.

**SEHEMU B (Alama 40)**

Jibu maswali **yote** katika sehemu hii.

11. Kwa kutumia hoja tano, fafanua namna mwalimu anavyoweza kujenga ubunifu na udadisi kwa wanafunzi kwa kuwashirikisha katika uandaaji wa zana.
12. Pendekeza mambo matano ya kuzingatia wakati wa uandaaji wa zana kwa ajili ya kushiriki mashindano ya zana za kufundishia na kujifunzia katika wilaya ili shule iweze kushinda.
13. Chambua zana sahihi za kuwafundishia wanafunzi wenye changamoto ya ulemavu wa uoni hafifu, wasioona, wasiosikia, matatizo ya matamshi na wasioongea kabisa (bubu).
14. Eleza hatua tano utakazotumia kuwaongoza wanafunzi wa Darasa la Sita kuchora ramani ya Afrika ardhini.


Find this and other free resources at: https://maktaba.tetea.org